JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA
SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS

MKUU WA SHULE
Simu: (+255) 766089787
(+255) 755370998
Email:songeaboys50@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS,
S. L. P 2,
SONGEA.
01/12/2022

Unapojibu tafadhari taja; /
Kumb. Na. SSS.N.2/VOL.VI .....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI SONGEA BOYS' JAN. 2023

Natumia nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri mtihani wa darasa la saba. Na kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule sekondari ya Songea Boys'. Shule hii ipo katika mji wa Songea, Mkoa wa Ruvuma, umbali wa kilometa kumi na mbili (12) kutoka stendi kuu na ukifika stendi ya basi unaweza kuchukua **"TAXI" kwa gharama isiyozidi Tshs 15,000/= au pikipiki kwa nauli ya Tsh. 10000/=. Pia unaweza kutumia daladala hadi standi ndogo ya mjini Tshs 1000 kisha daladala tena hadi songea boys Tshs 500, au bajaji Tshs 700 au pikpiki Tshs 1500.**

Songea Boys ni shule ya bweni kwa wavulana tu. Shule itafunguliwa tarehe **06/01/2023.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **26/01/2022**. Baada ya hapo hutapokelewa. Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo: -

- **Form na: 1** Fomu ya afya (requesting for medical examination). Apimwe hospitali na mganga mkuu wa wilaya/mkoa kuhusu afya yake.
- **Form na: 2** Orodha ya mahitaji ya muhimu ya shule
- **Form na: 3** Kukubali nafasi uliyochaguliwa katika shule ya Songea Boys
- **Form na: 4** Sheria za shule. Tafadhali sana soma kwa makini kabla wewe na mzazi/mlezi wako hamjasaini fomu hiyo

Kumbuka kuwa kila mwanafunzi anapaswa kujaza fomu zote kikamilifu na kuzirejesha hapa siku atakayo ripoti. Hakikisha kila hitaji la usajili limekamilika kabla ya siku ya usajili. Pia siku 20 baada ya kufungua shule nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine, na wewe hautapokelewa. Mwisho ninakukaribisha na kukutakia mafanikio mema hapa shuleni

LUGOME G, G,
MKUU WA SHULE

The Headmaster
Songea Boys' Secondary School
P. O. Box 2
Songea

FOMU NO: 1

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical officer:

Fullname……

Age: ……. Years; sex:……..…

Blood count (red and white)……..……..…

Stool examination: ……..……

Urine analysis: ……..……..

Eye test: ……..…..

T.B test:……..……..

Ears: ……

Chest: ……..

Spleen: ……..……

Abdomen: ……..……

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical defects or important infections, chronic of family diseases, etc.

……

……

……

……

……

……

I certify that the above named candidate is fit to pursue his studies. Medical Officer' s.

Names:……

Designation: …… Signature: ……

Station: …… Date: ……

NOTE:

Medical Officer: At the time of examination of the individual/ particular student for any ailment please note

FOMU 2: MAHITAJI YA SHULE

A) SARE ZA SHULE

i. Surualimbili nyeusisiyo``less"zishonwe kwa unadhifu (Zisiwe zakubana)
ii. Shati nyeupe mbili za mikono mifupi. Mashati yatawekwa michoro ya utambulisho hapa Shuleni. Mashati lazima yawe na kola shingoni. Kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi watavaa shati nyeupe za mikono mirefu na kofia ya duara.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi, na soksi nyeusi jozi mbili.
iv. Sweta rangi ya bluu kwa vipindi vya baridi.
v. Nguo za michezo –bukta nyekundu, fulana ya bluu na raba nyekundu au nyeusi
vi. Nguo za kazi – kaptura ya kaki na fulana ya bluu. Nguo hizi lazima zivaliwe wakati wakazi **(majaketi, makoti, marapurapu na kofia haviruhusiwi).**
vii. Fulana- 01 (rangi ya kijivu) inunuliwe akishafika shuleni ili pasiwe na mchanganyiko wa rangi, aina na uwepo wa nembo ya shule.
viii. Tracksuit ya rangi bluu bahari (light blue)

NB: Swala la mashono kwa sare za shule kwa watakao kuja kushonea huku shule (suruali na sweta) wasiliana na 0766980470

B) MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

1. VIFAA VYA DARASANI
- Daftari za kutosha walau 10 (msomi)
- Countersbooks walau 10
- Kalamu za wino na mkaa za kutosha
- MKEBE wa hisabati (mathematical sets)
- Kamusi (dictionary)

2. VIFAA VYA BWENINI
- Ndoo - (1) (lita 20)
- Godoro (ft 2½)
- Mto na foronya
- Mashuka mawili (2) ya Rangi ya Pink na blanket (1)
- Chandarua yenye umbo la mstatili **(sio duara)** ya rangi ya bluu-(1)
- Kiwi
- Sabuni za kutosha za kufulia na kuogea
- Nguo za ndani
- Dawa za meno na miswaki
- Mafuta ya kupaka

3. VIFAA VYA BWALONI
- Kikombe -(1)
- Sahani-(1)
- Bakuri-(1)
- Kijiko-(1)

4. MAHITAJI BINAFSI

- Aje na fedha za kumtosha kwa ajili ya matumizi yake binafsi akiwa hapa shuleni, na itunzwe ofisi ya mkuu wa shule.

- **Anashauriwa ajiunge na bima ya afya hapa shuleni ambayo gharama yake ni 50400/= kwa kila mwaka. Ikumbukwe suala la afya ni nyeti katika kujifunza, Haswa kwa mtoto huyu aliyeko mbali na mzazi. Na kila asiye na bima ahakikishe analipia bima hiyo.**

NB: KWA KUONDOA USUMBUFU WA KUSAFIRI NA MIZIGO: VIFAA NA MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI (MFANO, GODORO, COUNTERBOOKS, DAFTARI, RIMU, SABUNI, NA VINGINE VILIVYO ORODHESHWA HAPO JUU) VINAPATIKANA KATIKA **DUKA LA SHULE**. Hivyo unaweza kuja na fedha kwaajili ya kupata mahitaji yako hapa shuleni)

ORODHA YA MAHITAJI MUHIMU YA SHULE NA GHARAMA ZAKE HAPA SHULENI

1. Daftari za msomi – 700/-
2. Peni-200/=
3. Pencil-200/=
4. Rula-500/=
5. Mathematical set-2000/=
6. Dictionary -15000/=
7. Ndoo-7000/=
8. Godoro -30000/=
9. Mto na foronya- 5500/=
10. Mashuka- 10000/=
11. Chandarua- 10000/=QA 3
12. Kikombe- 500/=
13. Containers- 2500/=
14. Kijiko- 500/=
15. Kiwi- 1000/=
16. Sabuni mche- 2000/=
17. Dawa ya meno – 500/=
18. Mafuta ya kujipaka- 500/=
19. Counterbook Q1-1600/=
20. Counterbook Q2- 2500/=
21. Counterbook Q3- 3000/=
22. Counterbook Q4- 4000/=

FOMU NA:3 KUKUBALI NAFASI ULIYOCHAGULIWA KATIKA SHULE YA SONGEA BOYS

.....

.....
Tarehe: .....

Mkuu wa Shule ,

Shule ya Sekondari Songea Boys'

S. L. P. 02,

SONGEA.

YAH: KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

Mimi .....
.....ninakujulisha kuwa **NIMEKUBALI/NIMEKATAA (kata isiyo husika)** KUJIUNGA NA SHULE YA SONGEA BOYS

KWA ALIYEKUBALI NAFASI:

Baada ya majadiliono na mzazi/mlezi wangu, tumekubaliana kuwa nitazifuata sheria za shule kama zilivyo ainishwa na kwamba endapo nitakaidi kufuata taratibu za shule basi hatua za nidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

KWA ALIYEKATAA NAFASI:

Baada ya majadiliano na mzazi/mlezi wangu tumekubaliana kuwa nafasi hiyo hatuitaki na kwamba itolewe kwa mwanafunzi mwingine wa **AKIBA**

KWA ALIYE KUBALI/KUKATAA: (kata isiyo husika)
JINA LA MWANAFUNZI: .....
SAINI YA MWANAFUNZI.....
JINA LA MZAZI/MLEZI.....
SAINI YA MZAZI/MLEZI.....
TAREHE .....

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAELEZO BINAFSI YAMHUSUYO MWANAFUNZI

A:TAARIFA ZA WANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.....

2. Tarehe ya kuzaliwa.....

3. Mahali alipo zaliwa (wilaya).....(Mkoa).....

4. Dini..... Dhehebu.....

B:TAARIFA ZA MZAZI /MLEZI

1. Jina la mzazi/mlezi anaye kutunza.....

2. Kazi ya Mzazi/Mlezi.....

3. Anuani/simu ya mzazi/Mlezi.....

4. Mahali ambapo anapoishi Mzazi/Mlezi - Kijiji/mji: ……..…..……..…….
   Kata.....

C:MAJINA YA NDUGU WENGINE WAWILI WANAO HUSIKA NA MALEZI YA MWANAFUNZI HUYO.

(Ni vyema wakiwa na uwezo wa kufika shuleni kila watakapohitajika)

1. Ndugu: .....

Anuani yake:.....

Namba ya simu: .....

2.Ndugu: .....

Anuani yake: .....

Namba ya simu: .....

D:TAARIFA ZA SERIKALI YA MTAA ANAKOTOKA MWANAFUNZI

Anuani za ofisi ya katibu kata au mwenyekiti wa mtaa/kijiji ambako mzazi /mlezi wa mwanafunzi anaishi.

1. Jina la mtendaji wa kata.....
   Kata ya .....Anuani.....

   Namba ya simu.....

2. Jina la Mwenyekiti wa mtaa/ kijiji..... ....
   Kijiji/mtaa-cha/wa .....Anuani.....
   .....

   Namba ya simu.....

FOMU NA:4 SHERIA ZA SHULE

Shule ni mahali ambapo kijana hujipatia elimu kwa mategemeo ya kujitayarisha kwa maisha yake ya leo na baadae. Anategemea kutumia uwezo wote kujiendeleza kielimu (maarifa ya kukabiliana na mazingira) kinidhamu, utii na vile vile kuishi vizuri katika jamii ndani na nje ya shule. Ili kuhakikisha kuwa lengo hilo linafanikiwa, **SHERIA ZA SHULE** zimewekwa. Sheria hizi ni muhimu kwa sababu zina jukumu kubwa la kulinda haki, utu wa kila mwanafunzi na sifa nzuri ya shule.

Walimu na wafanyakazi wasio walimu wote ni viongozi na walezi wa wanafunzi shuleni. Kila mmoja anawajibu wa kuhakikisha kuwa maisha ya kila mwanafunzi yanakuwa mazuri shuleni na badae. Nia ya shule ni kujenga busara ya kushika madaraka, kutii sheria na kutovunja ahadi, ushirikiano na hisani kisha kumuendeleza kitaluuma kila mwanafunzi darasani. Shule itamlea kila mwanafunzi na kumkuza katika misingi ya jamii katika hali yake ya uhuru, utu, usawa na kuthamini wengine katika jamii yake ndani na nje ya shule.

Hivyo utamtathimini mtu baadae siyo kwa sababu ya elimu yake tu, bali kwa matendo yake mazuri na imani yake. Ili kumpatia mwanafunzi misingi hiyo katika maisha yake ya baade, anapaswa kuzingatia sheria za shule kama ifuatavyo: -

1. **Kila mwanafunzi** anapaswa kutumia akili zake za asili na busara katika kufanya uamuzi wa vitendo mbalimbali shuleni na nje ya shule, kama kutohudhuria darasani au kuongea lugha ya matusi ni makosa makubwa.
2. **KUWAHI:**
   a) Kila mwanfunzi anapaswa kuwahi kuamka asubuhi na kufanya usafi wa mazingira na mahali anapolala pia kuwahi kwenye paredi saa 1:00 asubuhi hivyo kuchelewa ni kosa.
   b) Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi kwenye eneo la paredi “Assembly ground” kila inapogongwa kengele
   c) Kila mwanafunzi lazima awahi (kukimbia) anapoitwa na kiongozi (mwalimu, mfanyakazi au kiranja).
3. **HESHIMA**

Wanafunzi wanapaswa kuheshimiana wenyewe na kumheshimu mtu yetote anapokutana naye au kumkuta sehemu yoyote.

4. **UTORO**

Ni kosa kwa mwanafunzi kutoroka shule,darasani wakati ule anapokuwa shuleni/darasani kwa hiyo asitoke nje ya shule bila kibali (ruhusa)toka kwa mwalimu wa zamu.

1. SIMU

Simu haziruhusiwi na nikosa kwa mwanafunzi kumiliki simu au kutumia simu pasipo ruhusa. Simu zote zikabidhiwe kwa mkuu wa shule pindi mwanafunzi anapofika shuleni- atarejeshewa siku ya kufunga shule.

2. UTUNZAJI WA VIFAA VYA SHULE

NI kosa kwa mwanafunzi yeyote kuharibu mali ya shule kama vile; vitabu, viti, madawati n.k ikibainika **ITABIDI AFIDIE GHARAMA ZA MATENGENEZO AU UNUNUZI WA KIFAA KIPYA.**

3. WIZI

Ni kosa kwa mwanafunzi kuiba kushiriki katika kitendo cha wizi hata kikiwa kidogo.

4. UTULIVU NA AMANI

a) Ni kosa kwa mwanafunzi kupiga kelele akiwa darasani au hata nje ya darasa katika mazingira ya shule.
b) Ni kosa kwa wanafunzi kugombana au kuchochea ili wengine wagombane.
c) Ni kosa kwa wanafunzi kufanya mgomo au kushiriki katika aina yeyote ya mgomo.

Kazi ni wajibu wa kila mwanafunzi, kwa hiyo ni kosa kwa mwanafunzi kutofanya au kutegea kazi za mikono ambazo zitakuwa zimepangwa na viongozi ama walezi wako (wafanyakazi wa Songea Boys).

9. TAALUMA;

NI kosa kubwa kwa mwanafunzi, kutohudhuria vipindi na kutofanya mitihani ya ndani (terminal test) na mazoezi yoyote yatolewayo na walimu wa masomo darasani.

10. ULEVI NA UVUTAJI

a) Ni kosa kwa mwanafunzi kuvuta /kuuza sigara, bangi na kunywa aina yoyote ya pombe.
b) Ni kosa kwa mwanafunzi kuonekana akizurula kwenye maeneo ya nyumba za wageni (guest houses) na mabaa ya pombe.

11. UASHERATI

Ni kosa mwanafunzi kujihusisha na vitendo vya uasherati na iwapo mwanafunzi (mvulana) atasababisha mwanafunzi mwezake (msichana) kupata mimba au kumpa mimba msichana yoyote atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe .

12. MIPAKA YA MWANAFUNZI

Ni kosa kwa mwanafunzi kuonekana kwenye nyumba za walimu au wafanyakazi wasio waalimu bila ruhusa ya mkuu wa shule. Lakini pia ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya eneo la shule pasipo kibali cha kufanya hivyo (Kibali hicho kitatolewa na mwalimu wa zamu ama ofisi ya mkuu wa shule).

13. UTU NA THAMANI YA SHULE

Ni kosa na marufuku kwa mwanafunzi kufanya vitendo viovu vinavyoweza kudhalilisha ama kushusha heshima na kuleta sifa mbaya kwako binafsi, kwa mwanafunzi mwenzako na kwa shule.

N. B MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI;

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi,uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Makosa ya jinai.
5. Kupiga au kupigana.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma /shule
7. Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
10. Kushiriki kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kumiliki na /ama kutumia simu shuleni..

LUGOME G.G
MKUU WA SHULE

The Headmaster
Songea Boys' Secondary School
P. O. Box 2
Songea